76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

SOMO LA TATU

# KATIKA "TUIJUWE NJIYA YA WOKOVU"

## KWA KUJIFUNZA NA KUTII NENO LA MUNGU KWA KUTARAJIA UZIMA WA MILELE

**Utangulizi**

*Mpendwa katika Kristo, ufuatao ni mfululizo wa masomo manane ambayo imeandaliwa kwa wakristo walio na nia ya kujuwa mambo ya muhimu kuhusu wokovu (kuufikiya na kuulinda) kwa nia ya kuepuka maangamizi ya milele inayotarajiwa kwa wale wasiojali neema kubwa Mungu alitupa kwa njiya ya Yesu Kristo.*

*Masomo haya yana mada zifuatazo:*
Somo la 1: Maisha bila Kristo
Somo la 2: Wokovu kwa njiya ya Kristo
Somo la 3: Mamlaka ya Kristo
Somo la 4: Imani katika Kristo
Somo la 5: Toba kwa jina la Kristo
Somo la 6: Ubatizo katika Kristo
Somo la 7: Kanisa la Kristo
Somo la 8: Maisha mapya katika Kristo

*"Na Filipo alienda mahali alipo na kumsikia yule mtu anasoma kitabu cha nabii Isaya. Filipo akamwuliza, "Je, unaelewa maneno hayo unayoyasoma?" Yule towashi akasema, "Nitawezaje kuelewa pasipo mtu kunifafanulia?" Hivyo akamsihi Filipo ili apande na kuketi pamoja naye"* (Mdo. 8:30-31).

*"Hivyo kwa mwaka mzima Barnaba na Sauli wakakutana na kanisa na kufundisha idadi kubwa ya watu. Ilikuwa ni katika kanisa la Antiokia kwa mara ya kwanza wanafunzi waliitwa 'Wakristo.'"*(Mdo. 11:26).

*"Lakini baadhi yao kwa ukaidi walipokataa kuamini na kukashifu ujumbe wake mbele ya umati wa watu, Paulo aliachana nao, akawachukua wanafunzi na kuhojiana nao kila siku katika darasa la mtu mmoja aitwaye Tirano"*(Mdo 19:9).

*"Watu hawa walikuwa wema kuliko wale wa Tesalonika, kwa sababu walipokea Neno kwa nia iliyokuwa tayari kabisa, wakatafuta Maandiko kila siku kujuwa hakika ya maneno yale (waliofunzwa)"* (Mdo. 17:11).

*Mungu akubariki na kukuumbiya imani safi, juhudi na moyo wa utiifu kwa haya unayoyasoma.*

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

# Somo la tatu: Mamlaka ya Kristo.

Tunatoka soma katika somo la pili kwamba wokovu wapatikana kwa njiya ya Yesu Kristo tu. Basi, Yeye ana mamlaka gani na ameyapata wapi hata tumuamini yeye peke yake?

Tunapokubali Injili ya Kristo kama nguvu za Mungu kwa ajili ya wokovu (Rum.1:16), hatutaelewa kikamilifu ukweli wake bila kuzingatia kabisa ukubwa wa mamlaka ya Kristo. Ikiwa watu wanataka kufikiya neema ya Mungu, kufurahia wokovu kwa njia ya damu ya Yesu Kristo, ni lazima kabisa kukubali mamlaka makubwa ya Kristo, wasikiye sauti yake na kutii mapenzi yake. Ni vigumu kutambua Yesu kama mwokozi wa ulimwengu bila kuhakikisha pia kwamba yeye ni Hakimu mkuu wa Mungu na anahukumu mambo yote katika ufalme wake. Mamlaka halisi ya Kristo imetiwa sana mkazo katika maandiko mengi ya Biblia. Fikiria, kwa mfano, Waraka kwa Waebrania, sura ya 1 mistari ya 1 na 2 "*Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, **lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe**, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu*". Kulikuweko na wakati watu walipata kujuwa mapenzi ya Mungu wakitii mamlaka na maagizo ya Musa pia manabii ambao kwa njia yao (Musa na manabii), Mungu alisema "mara kadhaa kwa njia mbalimbali"; lakini kwa sasa, anazungumza nasi/nawe kwa njia ya Yesu Kristo tu. Angalia Yohana 1:17.

Musa alipotabiri kuja kwa Yesu Kristo, alisema: "*BWANA Mungu wenu atawainulia nabii kama mimi kutoka miongoni mwa ndugu zenu wenyewe. Lazima <u>mumsikilize Yeye</u>.*" (Kumbukumbu la Torati 18:15). Angalia Matendo 7:37.

Tunaposoma Mathayo 17:1-8, tunasikiya jinsi anafafanua ukweli kuhusu kugeuzwa sura kwa Yesu. Musa na Eliya walionekana wakiongeya naye wakati huo huo: wa kwanza aliwakilisha Sheria ya Agano la Kale, na wa mwisho aliwakilisha unabii wote wa Agano la Kale. Aya ya 5 inasema: "*Petro alipokuwa angali ananena, ghafula, wingu linalong'aa likawafunika na sauti ikatoka kwenye hilo wingu ikisema, "Huyu ni mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye sana, <u>msikilizeni Yeye</u>.*" Amri hii ya Mungu kwa kusikiliza Yesu waliipewa kwa kutazamia kusulubishwa na karibuni tu kufufuka kwa Mokozi, na badaye tu, mamlaka yake kuweko badala ya sheria ya Musa na manabii.

Soma Wagalatia 3:19; 24-25; Wakolosai 2:14; Waebrania 8:7-13; 10:9-10.

Leo, haiwezekani kufanya mapenzi ya Mungu kwa kufuata sauti ya Musa na Manabii katika Agano la Kale. Lazima kusikiliza sauti ya Kristo, ambaye sheria yake yapatikana katika Injili ya Agano Jipya. Inatupasa tujuwe wazi kwamba kukana mamlaka ya Kristo, ni kukana hapohapo mapenzi ya Mungu (Luka

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

10:16), lakini kutii mapenzi ya Mungu yanayojulikana kwa njiya yake (Yohana 7:16; 17:4-8 ).
Baada ya ufufuo wake na kabla ya kupaa kwake kwenda mbinguni, Bwana alisisitiza rasmi kuhusu mamlaka yake makubwa akisema : "*Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani*" (Mathayo 28: 18).

***Swali***: Basi ni mamlaka gani aliyo nayo mbinguni na katika dunia?
***Jibu***: Mamlaka yote?

Kwa hiyo, hakuna lolote litakalokuwa kweli, kamilifu na la kiMungu katika dini (mambo yote inayoelekeya imani) ikiwa hailingani na mamlaka ya Kristo. Kwa kufuata na kutii mamlaka ya Kristo, watu hupata chochote wanachohitaji kujuwa na kufanya ili kuufikiya wokovu upatikanao katika Kristo peke yake pia kwa kuyatengeneza maisha yao siku kwa siku mbele za Mungu ili kutarajia uzima ujao (wa milele). Soma Yohana 6:68-69; 17:3; 2 Petro 1:3.

Mamlaka makubwa ya Yesu Kristo imewekwa mkazo sana kufuatana na nafasi yake ya juu sana ambayo amepewa na Baba wa mbinguni. Paulo anasema kuhusu nguvu ambazo Mungu "*alizitumia alipomfufua Kristo kutoka kwa wafu, akamketisha mkono Wake wa kuume katika mbingu, juu sana kuliko falme zote na mamlaka, enzi na milki na juu ya kila jina litajwalo, si katika ulimwengu huu tu, bali na katika ule ujao pia. Naye Mungu ameweka vitu vyote viwe chini ya miguu Yake na amemfanya Yeye awe kichwa cha vitu vyote kwa ajili ya Kanisa, ambalo ndilo mwili Wake, ukamilifu Wake Yeye aliye yote katika yote".* (Waefeso 1:20-23). Soma tena Wafilipi 2:8-11, Wakolosai 2:9-10, 1 Petro 3:22.

Ili tuelewe kikamilifu utawala mkuu wa Kristo, inabidi tumuone yeye kuwa ni: Mungu (Yohana 1:1), Nabii (Kumbukumbu la Torati 18:15: Matendo 7:37), Mfalme (1 Timotheo 6:14-15), Kuhani mkubwa (Waebrania 7:23-28, 8:1-5), Mwokozi na Mkombozi (Tito 2:13-14), nk. Tunapo hakikisha nafasi yake hii ya juu sana, ni nani tena anaweza tena kukana mamlaka yake? Isipokuwa mpinga-Kristo tu!

Wakati tunapokubali mamlaka ya Kristo, hapohapo tunasikia si Baba tu; ila pia, kama vile tunatoka kusoma hapo juu, mitume wa Kristo. Kutupilia mbali mafundisho ya mitume, ni kupuuzi pia mamlaka ya Kristo. Angalia Luka 10:16. Mitume walikuwa mashahidi wa Bwana duniani, na hao walisema yote yaliyo yake. Aliwaambiya: "*Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi kote na Samaria, hadi miisho ya dunia*" (Matendo 1:8). Mtume Paulo alisema: "*Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Kristo, kana kwamba Mungu anawasihi kwa kupitia vinywa vyetu, nasi twawaomba sana ninyi kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu"* (2 Wakorintho 5:20). Yohana, akizungumza kwa ajili yake mwenyewe na mitume wengine wote, alisema: "*Sisi twatokana na Mungu na ye yote anayemjua Mungu hutusikiliza, lakini asiyetokana na Mungu hatusikilizi. Hivi ndivyo*

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

*tunavyoweza kutambua Roho wa Kweli na roho ya upotovu"* (1 Yohana 4:6). Soma 1 Yohana 1:1-4.

Tunapotega sikio kwa maneno anayotuambiya Kristo, tunasikiliza pia Roho Mtakatifu. Kabla ya kumaliza huduma yake hapa duniani, Yesu aliahidi kutuma Roho Mtakatifu kwa mitume. Yeye alipashwa shuhudia Kristo na kuwakumbusha na kuwafunza wao juu ya mambo Yesu aliwafundisha ili mitume waweze kuhubiri Kristo na mafundisho yake kwa watu. (Yohana 14:26, 15:26-27, 16:13). Kwa kutoa ushahidi juu ya mamlaka na nguvu ya wokovu wa Yesu pia kujulisha mapenzi ya Mungu kwa watu kwa njia ya mitume, Roho Mtakatifu atasibitisha mbele ya ulimwengu kuhusu dhambi, haki na hukumu (Yohana 16:7-11). Lazima tusisitize hapa kuwa, Roho Mtakatifu alipoongoza mitume, alionyesha daima mamlaka na utukufu wa Kristo: "*Atakapokuja huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie katika kweli yote. Yeye hatanena kwa ajili Yake mwenyewe, bali atanena yale yote atakayosikia, naye atawaonyesha mambo yajayo. Atanitukuza Mimi, kwa maana atayachukua yaliyo Yangu na kuwajulisha ninyi"* (Yohana 16:13-14). Wao ndio wamelitolea Kanisa mafundisho ya msingi kutokana na yale waliyopokeya kwa Bwana. "*Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii …*" (Waefeso 2:20). "*Kwa maana mimi nilipokea kutoka kwa Bwana yale niliyowapa ninyi…*" (1Korintho 11:23)

Tufikiriye basi nini kuhusu wale wanaodai kuwa walipokea Ishara za pekee (funuo zingine) za Roho Mtakatifu, ambazo ni zingine zingine zaidi ya Habari Njema ya Kristo? Wao ni waongo tu! Ufunuo wote uliotolewa na Roho Mtakatifu kupitiya watu waliovuviwa naye, umeandikwa katika Agano Jipya ambamo hupatikana neno na mamlaka ya Kristo. Wale ambao hufundisha au kutenda yasiyokuwa katika Agano Jipya, hawana Kristo. "*Mtu ye yote asiyedumu katika mafundisho ya Kristo, bali akayaacha, yeye hana Mungu. Ye yote anayedumu katika mafundisho ana Baba na Mwana pia*" (2 Yohana 9).

Kwa kuwa Yesu Kristo ndiye mwenye mamlaka kwa imani ya waKristo na tena yeye ni Mkombozi wa watu, ni lazima kutafuta katika mafundisho yake ni nini inatupasa kufanya kwa kuokolewa. Kati ya kufufuka na kupaa kwenda mbinguni, Yesu aliwapa mitume wake ile ambayo huitwa maarufu "<u>tume kubwa</u>" (la grande commission) ambamo amefunua wazi shurti kwa watu ili kuokolewa kupitiya Yeye. Kuna maelezo matatu ya makini, "*Kwa sababu hii, enendeni ulimwenguni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, nanyi wafundisheni kuyashika mambo yote niliyowaamuru ninyi. Hakika Mimi niko pamoja nanyi sikuzote, hadi mwisho wa nyakati. Amen"* (Mathayo 28:19-20). " *Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ye yote aaminiye na kubatizwa ataokoka. Lakini ye yote asiyeamini atahukumiwa*" (Marko 16:15-16). *"Haya ndiyo*

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

*yaliyoandikwa: Kristo atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka kwa wafu. Toba na msamaha wa dhambi utatangazwa kupitia Jina Lake, kuanzia Yerusalemu. Ninyi ni mashahidi wa mambo haya".*(Luka 24:46-48).

Tunapo jumlisha maagizo yote yaliyomo katika hili "tume kubwa", tunaona kwamba, ili waufikiye wokovu katika Yesu Kristo, wenye dhambi lazima wamuamini Yeye, na kutubu pia kubatizwa. Masomo yatakayofuata baadaye, yataeleza kwa urefu kuhusu kila moja ya shurti hizi. Yatosha kusema hapa kwamba, ikiwa watu wanataka kufikiya na kushangiliya wokovu, ni lazima wajisalimishe chini ya shurti alizozitowa Kristo. Mtu aki
kataa kukubali moja ya amri zake, atakuwa amekataa mamlaka ya Kristo na kwa hiyo hatarithi mbinguni.

Tusifikiri kwamba Yesu ana mamlaka kwa sasa tu, bali ni Yeye tena ndiye atakuwa na mamlaka halisi Siku ya hukumu. "Kama *vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake. Naye amempa Mwanawe mamlaka ya kuhukumu kwa kuwa Yeye ni Mwana wa Adamu"* (Yohana 5:26-27). Sheria itakayo tuhukumu itakuwa ni neno la Kristo: "*Yeye anaye nikataa, na asiyepokea maneno yangu, ana mumoja anayemuhukumu: neno nililosema, lile litamhukumu siku ya mwisho"* (Yohana 12 : 48). Basi vipi ilivyo vema zaidi, kwa kutafuta ukubali wa Hakimu mkuu Yesu Kristo hapo siku ya mwisho na kuwa na uhakika wa kuwa tumetimiza yote aliyotuamuru? Maana, kama sisi tukikataa Kristo kwa kutokupokeya na kutii neno lake, basi Yeye pamoja na maneno yake tutahukumiwa siku ya mwisho.

Kwa kumalizia, ni vema mwanafunzi (msomi aliye na niya ya kutenda) asome kwa makini na unyenyekevu Mathayo 11:28-30 na Ufunuo 3:20. Vifungu hivi vinatoa mwaliko bora na kamili wa upendo, uliotolewa na Yesu Kristo (mwenye mamlaka yote katika mambo ya imani safi) na unaoelekeya watu wote. *"Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi". "Tazama, nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu ye yote akisikia sauti Yangu na kufungua mlango, nitaingia ndani na kula pamoja naye,naye pamoja nami."*

Kwa kuwa Kristo ndiye mwenye mamlaka yote kutoka kwa Mungu, lazima tujenge imani yetu ndani yake. Hakuna mwingine awaye yote (malaika wala mwanadamu) aliyepewa mamlaka mbinguni na duniani. Mtu akichagua kufuata mwingine (mafundisho mengine) na kuacha Kristo, atakuwa amechagua

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

mwenyewe njiya ya mauti wala si uzima, ijapokuwa "*Uweza Wake wa uungu umetupa sisi vitu vyote tunavyohitaji kwa ajili ya uzima na utawa (uchaji wa Mungu), kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake na wema Wake mwenyewe*" (2Petro 1:3).

Yesu alisema: "*Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia Kwangu* » (Yohana 14 :6).

Tumekwisha soma yafuatayo yaliyotamkwa na Mungu mwenyewe: *"Huyu ni mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye sana, msikilizeni Yeye."* Hii ndiyo maana hakuna mwingine ambaye tutaamini kwa nia ya wokovu wa roho zetu isipokuwa Yesu Kristo. Somo litakalofuata (la inne), litatufunza kuhusu "imani katika Kristo".

✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✩✩✩✩✩✩✩✩✩✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧

**Ikiwa una maswali yoyote wala kutaka mwangaza wa zaidi,**

✍Andikiya:

- Kanisa la kristo pa Bukavu, SLP/Po Box: 222, Cyangugu-Rwanda.
- Email: klk.bukavu@yahoo.fr

⇨ Kutana na watumishi wa Mungu pahali wanaposhiriki pamoja na kanisa kwenye anuani ifuatayo:
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – DRC.